

Muda: Saa 1 Dakika 40

KISWAHILI

SEHEMU YA A:

LUGHA

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu litaalo zaidi kati ya vale uliyopewa.

Ni jambo la 1 kuona uchafuzi wa mazingira unaondelea kufanyika nchini 2. Kwanza 3 miti iliyoko kwenye misitu yetu michache inaendelea kukatwa 4 kuwazia matokeo mabaya ya kitendo 5. Kitendo kama hiki kina hatari ya 6 kasi ya nchi hii kuwa 7 katika miaka ijayo.

- | | | | |
|-------------|----------------|---------------|---------------|
| A. | B. | C. | D. |
| 1. kutisha | 1. kutatiza | 1. kuogofya | 1. kukera |
| 2. yetu | 2. mwetu | 2. kwetu | 2. letu |
| 3. : | 3. ! | 3. , | 3. -- |
| 4. lichaya | 4. bighairi ya | 4. mbali na | 4. kinyume na |
| 5. hicho | 5. hiki | 5. hii | 5. hiyo |
| 6. kuongeza | 6. kuiongeza | 6. kuiongezea | 6. kuongezea |
| 7. kame | 7. mahame | 7. kavu | 7. jangwa |

Vijana wana 8 lao kwa taifa. Wewe kama mwanafunzi unaweza kuchangia maendeleo 9 hii kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli 10 shule. Ujibidiishe vilivyo, si katika masomo pekee. 11 pia katika michezo. 12 unaweza kushiriki katika shughuli za 13 taka katika mtaa ulio karibu 14 shule yako.

Ukifanya hivyo utakuwa 15 wito wa serikali kuhifadhi mazingira.

- | | | | |
|----------------|-----------------|------------------|-------------------|
| A. | B. | C. | D. |
| 8. kusudi | 8. wajibu | 8. lengo | 8. jukumu |
| 9. katika nchi | 9. kati ya nchi | 9. katika nchini | 9. kati ya nchini |
| 10. yote ya | 10. zote za | 10. lote la | 10. wote wa |
| 11. angalau | 11. ingawa | 11. bali | 11. japo |
| 12. Hakika | 12. Ama | 12. Labda | 12. Aidha |
| 13. kuzua | 13. kuzoa | 13. kyokota | 13. kukoka |
| 14. kwa | 14. kwenye | 14. na | 14. wa |
| 15. umeitikia | 15. unaitika | 15. umeitika | 15. unaitikia |

Kutoka swali la 16-30 chagua jibu sahihi kulingana na maelezo uliyopewa.

16. Chagua kivumishi cha pekee katika sentensi ifuatayo.

Mwenyewe alikila chakula hicho chote.

- | | |
|--------------------|-------------------|
| A. mwenyewe | B. chote |
| C. hicho | D. alikila |

17. Ni sentensi gani yenye 'kwa' ya kuonyesha kusudi au sababu

- A. Kufika kwa polisi kulimnusuru bwana yule
- B. Kufaulu kwangu kuliwatia moyo wengi kijijini
- C. Alipofika kwa msena wake alipumzika
- D. Kuhukumiwa kwa wizi wake kulimfaa

18. Eleza matumizi ya maneno yaliyochorewa mstari katika sentensi ifuatayo:
Mtu mzuri huonekana vizuri kwa uzuri wake.
A. kiwakilishi, kielezi, nomino
B. kivumishi, kiwakilishi, nomino
C. kivumishi, kielezi, nomino
D. kivumishi, kielezi, kiwakilishi

19. Ni ipi nomino fungamano kati ya zifuatazo:
A. ujanja B. marashi
C. mahakama D. mwananchi

20. Chagua sentensi iliyo katika wakati ujao hali timilifu.
A. Mchezo utakuwa umeanza mtakapofika
B. Musa atakuwa akiwasubiri stanmi
C. Soko litakapofunguliwa wachuuji watauza
D. Juma atakuwa akisoma mtakapowasili

21. Ni sentensi ipi sahihi?
A. Mwizi alimokuwa palikuwa na giza
B. Mwizi alipokuwa kulikuwa na giza
C. Mwizi alikokuwa mlikuwa na giza
D. Mwizi alimokuwa mlikuwa na giza

22. Ni methali ipi inatushauri tuthamini uhusiano wa kidamu
A. wema hauozi
B. mkono mmoja laulei mwana
C. ndugu mui heri kuwa naye
D. udongo uwahi ungali maji

23. Chagua usemi taarifa wa :
**"Nitaondoka kuelekea ughaibuni kesho."
Mgeni alisema.**
A. Mgeni alisema angeondoka kuenda ughaibuni kesho
B. Mgeni alisema angeondoka kuelekea ughaibuni siku iliyofuata
C. Mgeni alisema ataondoka kesho
D. Mgeni alisema angeondoka kuelekea ughaibuni siku iliyopita

24. Jaza pengo kwa kiunganishi sahihi :
Nimerejea haraka _____ sikumpata afisini.
A. madhali B. yamkini
C. yakini D. ghalibu

25. Ni sentensi gani iliyotumia kivumishi '-ingine' kuonyesha 'baadhi ya'
A. Wanafunzi wameongezeka shuleni, tunahitaji walimu wengine
B. Itabidi nimwajiri kijakazi mwingine, yule wangu ameacha kazi
C. Wanafunzi wengine hawakuwa na vitabu vilivyohitajika
D. Namtaka mwanafunzi mmoja, wengineo warudi darasani

26. Chagua sentensi ambayo ina matumizi sahihi ya 'ki' ya masharti.
A. Nilikataa kuwa kikwao
B. Akifika tutajuzwa
C. Kisigino chake kimevimba
D. Kigombe hicho hakikufa

27. Tambulisha ngeli za nomino hizi:
Nyasi, miwani, ugonjwa
A. U-I, I-ZI, U-YA. B. KI-VI, U-YA, U-U
C. U-ZI, U-YA, I-I D. U-ZI, I-I, U-YA

28. Mtu anayehamia nchi nyingine na kufanya makao yake ya kudumu ni
A. mzalendo B. kibaraka
C. mlowezi D. balozi

29. Nini wingi wa ukubwa wa:
Kichwa cha mtoto kimenyolewa
A. Majichwa ya matoto yamenyolewa
B. Vichwa vya watoto vimenyolewa
C. Majichwa ya watoto yamenyolewa
D. Jichwa la toto limenyolewa

30. Tambulisha sentensi iliyo na kiwakilishi cha a-unganifu.
A. Yule ni mwerevu B. Wa mama ni huyu
C. Changu kimeharibika D. Chote kimeliwa

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40

Uhuru ulikuwa mwingi katika chuo kikuu kinyume na shule ya upili na hata nyumbani. Wanafunzi walikuwa wengi katika darasa la mhadhiri na asingejua wanafunzi wake kwa majina. Pili hakukuwa na kazi ya kiamboni ya kila siku, na tatu kila mmoja alilala katika chumba chake. Kila mtu aliruhusiwa kutumia vileo mradi uwe ni wakati unaofaa na viwe vimeruhusiwa na serikali.

Kuna wale waliohudhuria mafunzo wakiwa mbali kwa kuwauliza wenzao wawatilie sahihi kwenye ratiba ya kuhudhuria. Wengine walisusia masomo na kusema kwamba wangesoma mtihani ukikaribia. Kuna wale waliokuwa na mifuko mizito waliofanyiwa kazi na mazoezi na wenzao kisha wakagharamia gange ile. Bendera alipojiunga na chuo kikuu baada ya kuchanganya mikono kwa miaka minne, alifurahi upeo wa kufurahi kujipata katika uhuru wa jinsi liyo. Alijiunga na kikundi cha walegevu na utepetevu. Mitihani ilipotangazwa kuanza, akaanza kukimbia huku na kule wakiwa wa wenzake. Walijaribu kuleta vijisababu vya kuahirisha mitihani ile lakini walikuwa wakiwashia vipofu taa.

Liwake lisiwake mitihani ilianza kama ilivyokusudiwa. Waliosoma walishusha pumzi na kukabiliana na mitihani ile kiume. Kwa upande mwingine, kiza la kaniki liliwagubika akina yahe wa masomo. Baada ya siku ile, mipango kabambe ilibidi ifanywe ili kujinasua na utando wa fedheha ya kuramba mchanga kwenye mitihani. Hapo mgomo wa dharura ukapangwa na rabsha ikazuka. Moja kwa moja uharibifu pamoja na uporaji wa mali ukaanza papo hapo. Magari ya wajenga nchi yalivamiwa kwa mawe na mengine kuteketezwa bila sababu. Bendera licha ya kuwa alikuwa kiokote wa kudhaminiwa katika masomo yake alikuwa nambari wahedi kutekeleza uovu ule. Baadaye chuo kikuu kilifungwa bila arifa na kila mmoja akapewa nusu saa awe amehama. Polisi wa kukabiliana na ghasia walifika na kuhakikisha kwamba amri ile ilitimizwa bila ulegevu. Vichwa maji waliamua kukabiliana na polisi bila kujua kwamba walikuwa wakichezea mapindi ya nyoka.

Walipata kichapo cha mwaka. Wengine katika pandashuka zile walilemazwa na kuumizwa vibaya. Hatimaye waliinua mikono na kuelekea makwao. Bendera alikuwa miongoni mwa wasiobahatika kwani alivunjika mkono. Baada ya kutoka hospitalini alielekea nyumbani hadi kwa mdhamini wake. Huko alifahamishwa kuwa aliyekuwa akiyadhamini masomo yake hangeweza kuendelea kumdhamini kwani gari lake na biashara yake ziliharibiwa wakati wa mgomo ule.

Bendera alilengwa na machozi mazito na kulia kilio cha shake. Alikumbuka jinsi alivyohusika kutekeleza uovu huo na kujiharibia maisha yake. Laiti angejua angetenda yaliyompeleka chuoni. Sasa anaishi maisha ya kitwea pekee. Anateseka na kulia, lakini ukiyavulia nguo maji huna budi kuyaoga.

- | | |
|--|---|
| <p>31. Ni jambo lipi halikuleta uhuru katika chuo kikuu ?</p> <p>A. Kutojulikana na wahadhiri</p> <p>B. Wanafunzi kuwa wengi</p> <p>C. Ruhusa ya kutumia vileo</p> <p>D. Kila mmoja kulala katika chumba chake</p> | <p>36. Akina yahe wa masomo ni nani katika taarifa hii?</p> <p>A. Waliogubikwa na kiza cha kaniki</p> <p>B. Waliosomea mitihani yao vizuri</p> <p>C. Waliokosa kusoma ipasavyo</p> <p>D. Waliokuwa wakiingia usiku kukiwa na giza</p> |
| <p>32. Taarifa hii haielezi kwamba</p> <p>A. kuna vileo haramu katika chuo kikuu</p> <p>B. si lazima kila mtu ahudhurie mafunzo</p> <p>C. katika chuo kikuu hakuna kazi ya kiamboni</p> <p>D. kuna wale husoma mitihani inapokaribia tu</p> | <p>37. Mgomo uliandaliwa kwa nini?</p> <p>A. Ili nafasi ya kusomea mitihani ipatikane</p> <p>B. Ili nafasi ya kupora na kuharibu mali ipatikane</p> <p>C. Ili wanafunzi wafukuzwe nyumbani</p> <p>D. Ili waweze kuepukana na mitihani</p> |
| <p>33. Ni kina nani walifanyiwa kazi na wengine?</p> <p>A. Waliokosa kufika darasani</p> <p>B. Waliolemewa na maswali</p> <p>C. Waliozembea kufanya kazi ile</p> <p>D. Waliozembea na kuwa na uwezo wa kuwalipa wenzao</p> | <p>38. Ni kweli kwamba</p> <p>A. mgomo uliofanywa usingeepukika</p> <p>B. uharibifu wa mali uliletwa kwa kuogopa kufeli mitihani</p> <p>C. polisi walikuja kutekeleza amri waliyotoa</p> <p>D. mali ya wananchi wote yaliharibiwa</p> |
| <p>34. Bendera alitoa mchango upi binafsi ili ajiunge na chuo kikuu ?</p> <p>A. Alidhaminiwa masomo yake na mdhamini</p> <p>B. Alizembea alipojiunga na chuo kikuu</p> <p>C. Alifanya bidii masomoni</p> <p>D. Alikimbia huku na kule na wenzake</p> | <p>39. Ni methali ipi haiwezi kutumika katika kisa hiki ?</p> <p>A. Mtegemea nundu haachi kunona</p> <p>B. Ajizi ni nyumba ya njaa</p> <p>C. Msiba wa kujitakia hauna kilio</p> <p>D. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe</p> |
| <p>35. Ni nini maana ya 'shusha pumzi' kama lilivyotumika ?</p> <p>A. Kuwa na utulivu</p> <p>B. Kupumua haraka na kuhema</p> <p>C. Kuwa na matatizo</p> <p>D. Kukumbuka majibu ya maswali</p> | <p>40. Maisha ya kitwea ni yapi ?</p> <p>A. Maisha ya taabu</p> <p>B. Maisha ya furaha</p> <p>C. Maisha ya upweke</p> <p>D. Maisha ya anasa</p> |

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Yalikuwa majira ya jioni siku ya Jumatatu wakati wa msimu wa baridi. Ingawa haikuwa saa moja, tayari giza la jioni lilikuwa limeshika huku na huku. Giza hilo liliongezwa na mawingu yaliyotanda angani mchana kutwa. Siku nzima ilifanana na mtu aliyekuwa amenuna, haikuonyesha furaha ya aina yoyote na jua nalo halikuonekana. Hali ya hewa iliyokuwako ilimvutia sana pwagu aliyeisubiri jioni hiyo kwa hamu kubwa. Tangu alipoyaaacha masomo yake yapata miaka minne iliyopita pwagu aliifurahia kazi yake mpya. "Mwanangu mambo unayoyafanya sio mazuri," alimkanya babaye. Pwagu hakuusikiliza wala kuuzingatia ushauri aliopewa na baba yake mzazi. "Mwanangu dunia hii ina matatizo makubwa na ukipanda mabaya utavuna majuto" alimshauri mama yake mzazi, lakini pwagu hakuusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini kwa kuamini kuwa aliweza kujiamulia la kufanya.

Siku iliyotangulia alifanya uchunguzi wake na kutambua kuwa jirani yao, Bwana Bidii alikuwa na hazina kubwa ya pete za dhahabu za mkewe Wema. Nia yake siku hiyo ilikuwa kutafuta njia ya kuingia katika nyumba ya bwana Bidii iliyokuwa kubwa na kuzitwaa pete hizo kwenda kuuza. Basi baada ya kujiandaa alitoka nyumbani kuelekea kwa Mzee Bidii. Aliufunika uso wake kizuizui ili asiweze kutambuliwa na yeyote wakati huo.

Alipofika yalipokuwa makazi ya Mzee Bidii, alitafuta mwanya wa kupenyeza. Sehemu aliyokuwa ameliona mchana ilikwa imezibwa kwa matawi ya miba. "Sasa ni nani aliyefanya hivi?" Alijiuliza Pwagu akienda huko na huko kutafuta mahali pengine. Kwa bahati nzuri aliweza kupata mahali pa kupitia na kuingia uwanjani. Alipotokezea uwanjani tu, alikumbana na jambo ambalo hakulitarajia. Alisikia mbwa aliyebweka kwa sauti ya juu sana. "Mbona mbwa wa Bidii niliyemtilia sumu wiki iliyopita akafa jana, sasa huyu ametoka wapi?" Alijiuliza akirudi kinyumenyume.

Alijigonga kwenye kisiki kilichokuwa nyuma yake na kuanguka chini. Wakati huo yule mbwa alikuwa akimkimbilia na kubweka kwa sauti ya juu kabisa. Pwagu hakuwa na wakati wa kusimama ila kununua pujo mguu niponye. Mzee Bidii na wanawe walitokeza wakati huo wakiwa na tochi kubwa iliyokuwa na mwanga mkali kama wa mbalamwezi. Walimshika Pwagu na kumfunga kwa kamba halafu Mzee Bidii akalivasha gari lake wakampeleka kwenye kituo cha polisi kilichokuwa karibu. Baadaye hukumu ilitolewa. Pwagu alipatikana na hatia na akafungwa jela miaka ishirini. Pwagu hakujua maana ya methali, asiye funzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu hadi siku hiyo.

- | | |
|--|--|
| <p>41. Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa kifungu</p> <p>A. Pwagu alimaliza masomo yake yapata miaka minne iliyopita</p> <p>B. Yalikuwa majira ya jioni msimu wa vuli</p> <p>C. Giza la jioni liliongezwa na mawingu yaliyotanda angani mchana kutwa</p> <p>D. Baba yake pwagu alikuwa mkwasi</p> <p>42. 'Ukipanda mabaya utavuna majuto' ina maana kuwa</p> <p>A. ukifanya mabaya utalipwa fadhila</p> <p>B. anayefanya mabaya hujidhuru yeye mwenyewe</p> <p>C. wema hulipwa na wema</p> <p>D. mabaya na majuto ndio ulimwengu</p> <p>43. Kulingana na aya ya tatu lengo la Pwagu lilikuwa</p> <p>A. kuelekea kwa mzee Bidii kuzitwaa pete za dhahabu na kuziua</p> <p>B. kununua pete za dhahabu</p> <p>C. kuazima pete za mke wa mzee Bidii</p> <p>D. kuitembelea jamaa ya mzee Bidii</p> <p>44. Aliufunika uso wake 'kizuizui' ina maana</p> <p>A. Alishikwa na kizunguzungu</p> <p>B. Alifunika uso wake kwa mikono miwili</p> <p>C. Aliyafumba macho yake ili asijulikane</p> <p>D. Alitumia kitambaa kufunika uso wake ili mtu asimjue</p> <p>45. Kulingana na kifungu, Pwagu alikuwa na hulka za aina gani?</p> <p>A. Alikuwa mwadilifu</p> <p>B. Alikuwa mwadhini</p> <p>C. Alikuwa msumbi</p> <p>D. Alikuwa msikivu</p> | <p>46. Ni zipi athari za kuwa lusu kwa mujibu wa kifungu.</p> <p>A. Kuishi maisha mema ya starehe</p> <p>B. Kujuta na kusunoneka daima</p> <p>C. Kuwa stadi na kuheshimiwa</p> <p>D. Kupewa mkono wa tahania na watu wengi</p> <p>47. Wazazi wa Pwagu walifanya nini kuhusu tabia na mienendo yake?</p> <p>A. Kumkanya aache tabia ya kuwa na mkono mrefu</p> <p>B. Kumuunga mkono pwagu katika shughuli zake</p> <p>C. Kumpongeza mwanao kwa ustadi wake</p> <p>D. Kumtelekeza Pwagu kwa ujeuri wake</p> <p>48. Kwa nini Pwagu alipigwa na butwaa kumsikia mbwa akibweka kwa sauti ya juu?</p> <p>A. Alikuwa amejificha mbwa asimwone</p> <p>B. Mbwa wa mzee Bidii alimjua jirani yake</p> <p>C. Alimpa minofu ili asibweke</p> <p>D. Pwagu alikuwa amemtilia sumu na akafa</p> <p>49. Msimu wa baridi ni kipupwe ilhali msimu wa mvua nyingi huitwaje?</p> <p>A. Mchoo</p> <p>B. Matlai</p> <p>C. Kifuku</p> <p>D. Vuli</p> <p>50. Chagua kichwa mwafaka au kinachofaa zaidi kwa kifungu hiki?</p> <p>A. Mpanda ngazi hushuka</p> <p>B. Asiyejiangalia huishia ningalijua</p> <p>C. Cha mlevi huliwa na mgema</p> <p>D. Chururu si ndondondo</p> |
|--|--|